

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

Telegram "AFYA", DODOMA
Nambari ya Simu: +255 026 – 2323267
E- Mail Na. ps@afya.go.tz



Mji wa Serikali Mtumba,
Barabara ya Afya,
S.L. P 743,
40478 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

UGONJWA WA KIFUA KIKUU WAENDELEA KUPUNGUA NCHINI

Dodoma, Jumatano, Mei 20, 2020

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, wazee na Watoto Mhe. Ummu Mwalimu amesema maambukizi ya Kifua Kikuu (TB) yamepungua nchini kutoka wagonjwa 164,000 mwaka 2015 hadi kufikia wagonjwa 142,000 mwaka 2018.

Waziri Ummu amesema hayo wakati akikabidhi Hadubini 57 kati ya 941 zilizonunuliwa na Serikali kwa ufadhili wa Global Fund, zikiwa na thamani ya Shilingi Bilioni 3.3, na zoezi hilo litakuwa endelevu zikiwa zimeanza kutolewa kwa mkoa wa Dodoma.

Pamoja na hayo Waziri Ummu ametumia muda huo kueleza mafanikio yaliyofikiwa na Mpango wa Taifa wa Kifua Kikuu na Ukoma ikiwa ni pamoja na kupungua kwa maambukizi mapya kwa asilimia 18 lengo likiwa ni asilimia 20 na vifo vimepungua kwa asilimia 27 lengo likiwa ni asilimia 35.

Aidha, Waziri Ummu amesema ugunduzi wa Kifua Kikuu unaendelea kuimarika ambapo idadi ya wagonjwa waliogundulika na kuwekwa kwenye matibabu imeongezeka kutoka wagonjwa 62,180 mwaka 2015 hadi kufikia 82,140 mwaka 2019.

Kwa upande wa **vituo vya ugunduzi wa tiba**, Waziri Ummu amesema katika kipindi cha miaka mitatu vituo vimeongezeka kutoka **vituo 662 mwaka 2016** hadi kufikia **vituo 1,201 mwaka 2019**.

Ameongeza katika kipindi hicho cha miaka minne idadi ya wagonjwa waliogundulika kuwa na Kifua Kikuu imepungua kutoka **wagonjwa 164,000 mwaka 2015** hadi **wagonjwa 142,000 mwaka 2018** huku vifo vinavyotokana na TB navyo vikipungua kutoka makadirio ya **vifo 30,000 mwaka 2015** hadi **vifo 22,000 mwaka 2018**.

Waziri Ummu Mwalimu amesema hadubini hizo zinazokabidhiwa zitapelekwa katika vituo vipya vya kutolea Huduma za afya 487 ambavyo vimejengwa, Hospitali za Mkoa 3, Hospitali za Wilaya 69 pamoja na vituo vya afya vya zamani 315 pia kubadilisha hadubini zilizoharibika katika vile vituo vyenye uhitaji.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Dkt. Binilith Satano Mahenge ameishukuru Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kutambua ulazima wa kuwepo kwa hadubini hizo katika maeneo mbalimbali ya kutolea

huduma za afya lengo likiwa ni kuondoa usumbufu kwa wananchi kusafiri umbali mrefu kutafuta huduma hiyo.



Gerard Julius Chami

**MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO YA SERIKALI
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO**